Kipeperushi hiki kimetayarishwa kama sehemu ya **Mpango wa Elimu kwa Mtumiaji wa Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya (CA).** Kina maelezo kuhusu usajili wa kadi ya SIM nchini Kenya.



## Swali la 1. Usajili wa mtumiaji ni nini?

Usajili wa mtumiaji ni mchakato wa kurekodi na kuthibitisha maelezo ya kibinafsi ya mtumiaji unaofanywa na mtoa huduma wa mawasiliano. Maelezo hayo ni pamoja na nambari ya simu, jina, tarehe ya kuzaliwa, jinsia, anwani (ya posta na/au anwani ya eneo) na nambari mbadala za simu kama zipo.

## Swali la 2. Kwa nini usajili wa mtumiaji ufanywe?

Usajili wa mtumiaji unalenga kulinda umma dhidi ya vitendo vya utovu wa usalama ikiwa ni pamoja na kueneza vitisho vinavyotolewa na magaidi, ulanguzi wa dawa za kulevya, utakasishaji wa fedha haramu, unyakuzi wa pesa, ulaghai, ujumbe wa chuki na uchochezi ambao kwa sasa umesambaa duniani. Kenya haiwezi kuthubutu kupuuza au kuachwa nyuma kwenye mipango inayolenga kuulinda umma dhidi ya shughuli kama hizo. Usajili wa kadi ya SIM unaongozwa na Agizo la Serikali lililotolewa tarehe 20 Julai 2009 na Sheria ya Habari na Mawasiliano ya Kenya (Kanuni za Usajili wa Kadi ya SIM), 2015 inayomtaka kila mtumiaji wa huduma ya mawasiliano nchini kusajili kadi zao za SIM.

## Swali la 3. Je, maelezo ninayotoa yanaweza kutumika kwa madhumuni tofauti na yaliyonuiwa?

Taarifa inayokusanywa itatumika tu kwa madhumuni yaliyofanya zoezi hili la usajili kufanywa na panapohitajika, maelezo hayo yanaweza kutolewa kwa mamlaka za kiserikali kadri inavyokubalika kisheria.

## Swali la 4. Je, maelezo yanayokusanywa wakati wa usajili wa mtumiaji yanatosha kwa ajili ya huduma zote zinazotolewa na mtoaji huduma?

Si lazima. Kila mtoa huduma atatoa ushauri kuhusu maelezo zaidi ya usajili kwa uandikishaji wa huduma/bidhaa zingine kila panapohitajika.

## Swali la 5. Ninawezaje kuthibitisha maelezo ya usajili wa kadi yangu ya SIM?

Mtumiaji anaweza kuthibitisha maelezo yake ya usajili kwa kuwasiliana na watoa huduma husika.

## Swali la 6. Je, usajili wa mtumiaji ambaye ni 'mtoto' utawezeshwa vipi?

Mtoto atahitaji kuandamana na mtu mzima aliye na hati muhimu za utambulisho ili kununua na kujisajili kama mmiliki wa kadi ya SIM. Mtoto huyo atasajiliwa tu kama mtumiaji wa kadi hiyo ya SIM. Pindi mtoto anapofikisha umri wa miaka 18, mtu mzima ambaye kadi hiyo ya SIM imesajiliwa kwa jina lake, atakuwa huru kubadilisha usajili ili uwe katika jina la huyo kijana, ambaye ukubalifu na maelezo ya utambulisho wake yatahitajika pia ili kutekeleza mabadiliko hayo.

## Swali la 7. Je, ninahitaji kutoa hati kwa ajili ya uthibitisho?

Kwa wananchi wa Kenya, hati yoyote kati ya zifuatazo (ZIKIWA ASILI) inahitajika: -

a) Kitambulisho asili cha taifa;
b) Pasipoti asili na halali;
c) Kitambulisho asili cha uanajeshi;
d) Cheti asili cha kuzaliwa

## Swali la 8. Ni hati zipi zinazohitajika kwa uthibitishaji kwa mtu asiye raia?

Wageni wanaotaka kusajili kadi zao za SIM watahitajika kuwasilisha hati yoyote kati ya zifuatazo (ZIKIWA ASILI): -

a) Pasipoti asili; au
b) Kitambulisho asili cha asiye raia.
c) Kitambulisho asili na halali cha taifa kilichotolewa (kwa wakaazi wa Afrika Mashariki)

## Swali la 9. Ni hati zipi zinazohitajika kwa uthibitishaji wa watumiaji ambao ni watu wanaowakilisha asasi na mashirika ya serikali?

Kwa watu wanaowakilisha asasi na mashirika wakilishi ya serikali, nakala zilizoidhinishwa za hati zifuatazo zitatumika katika uthibitisho:

a) Cheti cha Ushirikishwaji; au
b) Cheti cha Usajili; au
c) Sheria Inayofaa au ilani ya Gazeti

## Swali la 10. Je, data iliyokusanywa na mtoa huduma ni salama na ya siri kwa kiasi gani?

Mtoa huduma ana wajibu wa kuhakikisha kwamba maelezo yaliyokusanywa kutoka kwa watumiaji yamewekwa kwa njia salama, ya siri na kutoingiliwa. Maelezo yaliyokusanywa HAYATAFICHULIWA kwa mtu yeyote isipokuwa kama inavyokubaliwa na sheria yoyote iliyoandikwa. Nchini Kenya, Sheria ya Ulinzi wa Data ya 2019 inatumika.

Je, Umesajili Kadi Yako ya SIM_.pdf 2 06/09/2023 13:20

## Swali la 11. Ni nini hufanyika endapo umiliki wa laini ya simu utabadilika?

Mabadiliko yoyote kwenye umiliki wa laini ya simu yanapaswa kuripotiwa kwa mtoa huduma anayefaa ili kuwezesha kusasisha maelezo ya usajili wa kadi ya SIM. Uthibitishaji wa utambulisho wa mmiliki mpya pia utahitajika.

### *Unahitaji kufahamu zaidi*

Kwa habari zaidi kuhusu mada iliyopo hapo juu au sehemu nyingine yoyote ya afya na usalama wa mitambo ya mawasiliano, tafadhali wasiliana na:

COMMUNICATIONS AUTHORITY OF KENYA
*OPENING YOUR WORLD*

**Head Office**
CA Centre, Waiyaki Way, P.O. Box 14448, Nairobi 00800, Mobile: 0703042000,
Email: pea@ca.go.ke, info@ca.go.ke, Complaints: chukuahatua@ca.go.ke,
020-445 5555, 0714 455 555, 0737 455 555

**CA Western Regional Office**
1st Floor KVDA Plaza
P.O. Box 2346, Eldoret 30100
Mobile: 0703042105, Email: wro@ca.go.ke

**Central Regional Office**
Ground Floor, Advocates Plaza
P.O Box 134, Nyeri 10100
Mobile : 0703042181, Email : cero@ca.go.ke

**CA Coast Regional Office**
3rd Floor, NSSF Building
P.O. Box 8041, Mombasa 80100
Mobile: 0703042152, Email: cro@ca.go.ke

**Nyanza Regional Office**
2nd Floor Lake Basin Mall,
P.O Box 2016, Kisumu 40100
Mobile: 0703042130, Email: nro@ca.go.ke

Communications Authority of Kenya
@ca_kenya

***Ilani ya kujitoa hatarini***: Huku kila jaribio likiwa limefanywa ili kuhakikisha kuwa habari iliyojumuishwa katika hati hii ni sahihi, imekusudiwa TU kuwa kama mwongozo wa kuelekeza utendakazi salama wa mitambo ya mawasiliano na haipaswi kuchukuliwa kama (au kutumika badala ya) ushauri wa kisheria. Kwa hivyo,

Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya haitakubali kosa lolote kwa matokeo ya hatua zozote zilizochukuliwa, au maamuzi yaliyotolewa kwa misingi ya taarifa iliyotolewa.

**CA/PEA/CEP/KIS/F/3/2021**

COMMUNICATIONS AUTHORITY OF KENYA

www.ca.go.ke

# Je, Umesajili Kadi Yako ya SIM?

